# Faraja Health Training Institute

Email:info@farajahealth.ac.tz
Website:www.farajahealth.ac.tz
**+255 715 884 036**
**+255 673960289**
**+255622439955**
**+255762303379**

**Kumb.Na. FHTI/ADM/01/53**

**JINA LA MWANAFUNZI______________________________________________**

**ANUANI _______________________**

**Yah: KUCHAGULIWA KUANZA MAFUNZO YA STASHAHADA YA CLINICAL MEDICINE KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025**

Napenda kukuarifu kuwa umechaguliwa kijiunga na mafunzo ya stashahada ya Clinical Medicine (Diploma in Clinical Medicine). Mafunzo haya ni ya miaka mitatu, (3) na yanatarajiwa kuanza **14 Oktoba 2024**. Unatakiwa kufika chuoni kuanzia **14 Oktoba 2024** kabla masomo kuanza. Tarehe ya mwisho ya kupokelewa chuoni ni tarehe: **20 Oktoba 2024**, Baada ya tarehe hiyo mwanafunzi hatopokelewa.

Kuhusu gharama ya mafunzo, unatakiwa kulipa ada kiasi cha shillingi **Millioni mbili na Laki moja na Kumi na tano elfu tu (TZS. 2,115,000.00)** kwa mwaka wa kwanza. Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu NNE. Malipo yote ya Ada yanapaswa kufanyika kupitia akaunti ya benki **NMB Na.42910006885** Jina la Akaunti : **FARAJA HEALTH TRAINING INSTITUTE**.

*****Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi anayelipiwa ada.**

Mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni na uthibitisho wa malipo ya angalau na kiasi cha shillingi Laki Tano Elfu (500,000.00) cha Ada au Ada yote na mahitaji muhimu yote; la sivyo hatapokelewa kuanza masomo Kabla ya kuripoti chuoni, hakikisha umepimwa afya yako na daktari kwenye Hospitali au kituo cha Afya. Mara ufikapo chuoni, utamkabidhi Msajili wa Chuo Form ya uthibitisho wa Afya (Medical Examination Form) kutoka kwa daktari aliyekupima. Kukosa Form hiyo itakulazimu kujilipia kupimwa kwanza ndiyo upate usajili.Wakati wote uwapo chuoni, utatakiwa kutii sheria za nchi na za chuo. Ni sheria ya chuo kuwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza watalazimika kuishi hostel. Hii ni kwa maslahi yao ili watambue kwanza mazingira yao kabla ya kupangisha mitaani. Masuala yote ya mwanafunzi chuoni yatashughulikiwa na Uongozi wa chuo. Endapo kutakuwa na haja ya suala la mwanafunzi kushughulikiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Makao Makuu), jambo hilo litatakiwa kuwasilishwa kwanza kwa Mkuu wa Chuo na bodi ya Wakurugenzi ya Chuo kabla ya kupelekwa wizarani.

**UNATAKIWA KUFIKA CHUONI UKIWA NA MAHITAJI MUHIMU YAFUATAYO**: -

1. SARE ZA CHUO
   i. MWANAMKE
   - Magauni mawili (2) meupe ya mikono mifupi na urefu chini ya magoti isiopungua sentimita kumi (10cm).
   - Soksi nyeupe ndefu zinazofika magotini
   - Viatu vya rangi nyeusi vyenye visigino vifupi.
   - Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, na yawe marefu chin ya magoti; urefu usiopungua sentimita kumi (10cm).
   - Nguo za michezo T-shirt 2, bukta/suruali ya mazoezi (track suit) 2 na raba

   ii. MWANAUME
   - Suruali mbili (2) za rangi ya khaki
   - Mashati mawili rangi nyeupe mikono mifupi
   - Viatu vya rangi nyeusi na soksi nyeupe
   - Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, na yawemarefu chini ya magoti; urefu usiopungua sentimita kumi (10cm).
   - Nguo za michezo T-shirt 2, bukta/suruali ya mazoezi (track suit) 2 naraba

NB:

- ***Ni muhimu kuhakikisha kwamba mavazi yanatunza heshima yako na ya chuo, hivyo mavazi yasiwe ya kubana wala kuangaza kwa namna inayoonyesha maumbile ya mwili. Hata hivyo mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima wakati wote atakapokuwa chuoni. Sketi fupi na suruali za mlegezo ni marufuku kabisa.***
- ***Mwanafunzi hataruhusiwa kufika chuoni endapo akiwa na wigi (weaving hair), Nywele zenye Rangi, Kucha za bandia au Zilizopakwa Rangi Mchanganyiko , kusuka rasta au kunyoa Kiduku***

**SHERIA ZA TAASISI KWA UJUMLA**

- Taasisi inafuata sheria za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pia taasisi imejiwekea sheria ndogo ndogo katika mazingira yake ambazo mwanafunzi anapaswa kuzifuata.
- Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele, na wa kiume hawaruhusiwi kufuga ndevu
- Mwanafunzi anaweza kushindwa kuendelea na masomo au kufukuzwa shule kwa sababu zifuatazo:-
  - Akishindwa mitihani na ikiwa maendeleo yake hayaridhishi
  - Kushindwa/kutii sheria za taasisi ambazo atapewa na kutia saini pindi anapofika chuoni.
  - Kuonyesha tabia isiyoendana na maadili ya taaluma za afya.
  - Kushindwa kulipa ada kwawakati.
  - Sababu za kiafya ambazo zitamfanya asimudu masomo yake.

2. **MAHITAJI BINAFSI KWA USAFI**: -
   Ndoo 1 kubwa, Ndoo 2 ndogo, ufagio na mop
3. **VYETI / CHETI**: Cheti halisi (Original) cha kuhitimu F IV au F VI kinachotolewa na NECTA.

A: MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

| 1ST YEAR MUHULA WA KWANZA | | |
|---|---|---|
| **AWAMU** | **KIASI** | **MUDA WA MALIPO** |
| AWAMU YA KWANZA YA MALIPO | 500,000/= | ANAPO RIPOTI CHUO |
| AWAMU YA PILI YA MALIPO | 307,000/= | KABLA MTIHANI WA KWANZA (**CAT I)** |
| AWAMU YA TATU YA MALIPO | 250,500/= | KABLA YA MTIHANI WA PILI (**CAT II**) |
| JUMLA YA ADA **MUHULA WA KWANZA** | **1,107,500/=** | |
| HOSTEL | 175,000/= | |
| 1ST YEAR MUHULA WA PILI | | |
| **AWAMU** | **KIASI** | **MUDA WA MALIPO** |
| AWAMU YA KWANZA YA MALIPO + (ADA YA MTIHANI WA Wizara) | 500,000/= 150,000/= | ANAPO RIPOTI CHUO |
| AWAMU YA PILI YA MALIPO | 307,000/= | KABLA MTIHANI WA KWANZA (**CAT I)** |
| AWAMU YA TATU YA MALIPO | 250,500/= | KABLA YA MTIHANI WA PILI (**CAT II**) |
| JUMLA YA ADA **MUHULA WA KWANZA** | **1,207,500/=** | |
| HOSTEL | 175,000/= | |

MALIPO MENGINE

1. Ada kwa ajili ya Mitihani ya wizara ya afya (MoHCDGEC) Tshs 150,000/= unatakiwa kulipa katika akaunti ya chuo NMB Na.42910006885 malipo haya yalipwe tofauti na Ada ya masomo (**Slip yake Ijitegemee na Jina la Mwanafunzi lionekane**)
2. Ada kwa ajili ya malazi (Hostel Accomodation) **Tshs. 350,000**/= kwa mwaka nayo inajumuisha gharama za umeme, maji na ulinzi. au unaweza kulipa kwa muhula Tshs. 175,000/= kwa account ya NMB Na.42910006886, **Malipo haya hayapo ndani ya ada**.
3. ENDAPO wanafunzi atahitajika kufanya mtihani wa marudio (Supplementary Examination) atalipa Ada ya Tshs 50,000 kwa ajili ya kila mtihani huo anaopaswa kurudia.
4. Na ENDAPO mwanafunzi atatakiwa **kurudia Muhula wa masomo** atalipa nusu ya ada ya **mwaka husika**. Tunawashauri wanafunzi wasome kwa bidii na kuzingatia yale wanayofunzwa na Wakufunzi wao ili kukwepa adha ya hayo malipo

**NB:**

**Endapo tayari unayo bima ya Afya (iliyo hai) basi unatakiwa kuwasilisha kitambulisho chako cha bima kwa mhasibu na Afisa Mdahili wa wanafunzi (Admissions Officer) kwa uhakiki**

1. **Taarifa na hati muhimu unazotakiwa kuja nazo**:
   - Picha nne (4) passport size kwa ajili ya kumbukumbu za usajili
   - Vyeti halisi (original) vya kuhitimu kidato cha Nne n. k.
   - Cheti halisi (Original) cha kuzaliwa
   - Vitabu muhimu vya kozi husika pale inapowezekana .
   - Vifaa vya kuandikia kwa mfano madaftari (3 quire Register books 12), kalamu, rula n.k.
   - Mwavuli au koti la mvua na buti za mvua (gum boots)
   - Shuka 4, mto 1, blanketi 1, chandarua 1, taulo na foronya.
   - Blood Pressure Machine (sphygmomanometer)
   - Stethoscope
   - Patella hammer yenye sehemu ya kupima fahamu (pin and brush for testing sensation – touch na deep pain)
   - Koti jeupe la daktari la mikono mirefu na urefu wa kupitiliza magotiu cm 10 au zaidi
   - Kipimajoto cha nyuzi joto za Celsius (Centigrade scale thermometer)
   - Simu janja (Smart phone) - Android (Cell phone) yenye uwezo wa kupakua taarifa kutoka kwenye mtandao
   - Laptop aina yoyote na flash disc
   - Nguo za kujikinga baridi (koti/sweater)
   - Rim Paper 2 (1 Kwa kila Semister)

B. MALAZI

- Utapewa mahali pa kuishi. Kila chumba kina vitanda 4.
- Wanachuo watajitegemea kufanya usafi wa vyumbani.
- Kila Jumamosi kuanzia saa moja asubuhi hadi saa nne asubuhi ni siku ya usafi wa mazingira kitaifa na muda huo utatumika kufanya usafi mazingira ya bweni na chuo
- Malipo ya malazi yanaweza kulipwa kwa awamu moja au mbili kwenye akaunti ya chuo: **42910006886 NMB**. Mwanachuo atatakiwa kuwasilisha fomu halisi ya malipo kwa Mhasibu wa Chuo.



***Tafadhali lipa ada kwa wakati ili kuepuka usumbufu na msongo wa mawazo masomoni**

C. CHAKULA

- Mwanafunzi atajitegemea kwa chakula. Chuo kimezungukwa na migahawa ya wajasiriamali. Hata hivyo, jitihada zinafanywa kupata mkandarasi atakayeweza kutoa huduma ya chakula kwa gharama nafuu kwa wanafunzi katika eneo la Chuo
- Mwanafunzi yuko huru kupika mwenyewe Awapo Bwenini.

D. UCHELEWAJI.

- Tunakushauri uwahi siku ya kuanza shule, ukichelewa mtu mwingine atapewa nafasi yako baada ya wiki moja. Mwanafunzi atapata likizo ya wiki 4 kila mwaka na akichelewa baada ya likizo atalipa siku alizochelewa mara mbili katika likizo inayofuata.

  Kama kuna sababu maalumu (isiwe karo) mzazi atume taarifa chuoni, na kama ni ugonjwa mwanafunzi aje na cheti cha Daktari.

E. MSIBA.

- Ikiwa kwa bahati mbaya mwanafunzi atapata msiba, mzazi anatakiwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Taasisi na si mwanafunzi (mtoto wake) Mkuu wa Taasisi atamfahamisha mwanafunzi huyo aliyepata msiba. Mwanafunzi anaruhusiwa kwenda kwenye msiba kwa muda wa siku nne tu na ni kwa watu wafuatao:-
  a. Wazazi(Baba/Mama)
  b. Kaka na Dada
  c. Mtoto wake
  d. Mume/Mke

Kwa maswali, taarifa Zaidi tembelea tovuti yetu:
Website: www.farajahealth.ac.tz,
E – mail: farajahealth@yahoo.com au info@farajahealth.ac.tz
Au piga simu:

+255 715 884 036
+255 673960289 Afisa taaluma chuo cha afya faraja
+255622439955 Mkuu wa chuo cha afya faraja

+255762303379

Nakutakia kila la kheri katika mafunzo yako;

Dr. Elson Daud
MKUU WA CHUO,
FARAJA HTI

SEHEMU YA PILI

MAELEZO BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI

SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

a. Jina la mwanafunzi (majina Matatu)

………………………… …...…………………… ............................................

(JINA LA KWANZA) (JINA LA KATI) (JINA LA MWISHO/SURNAME)

b. Uraia ……………………………………………………………………………….

c. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………….

d. Shule aliyosoma kidato cha NNE……………………………………………

e. Shule aliyosoma kidato cha SITA …………………………………………….

f. Ulemavu wa kiafya………………………………………………………………

g. Ugonjwa wa kudumu…………………………………………………………….

h. Hali ya ndoa: Umeoa/umeolewa…………………haujaoa/haujaolewa………………

i. Malezi (wazazi wote wako hai) ………………………………………..

SEHEMU B (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

a. Jina la mzazi/mlezi (majina Matatu)

……………………… …...………………………………

......................................................

(JINA LA KWANZA) (JINA LA KATI) (JINA LA MWISHO/SURNAME)

b. Anwani ya mzazi/mlezi……………………..………………………………………………………..

c. Mahali anapoishi (kijiji/ kata/ mtaa)……………………………………………………………….....

d. Kazi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………………….

e. Mahali anapofanyia kazi ……………………………………………………………………………………….

f. Ndugu wawili wa karibu (wadhamini)

1. Jina……………………………………………………………………..

Anwani ......................................................................... namba ya simu ……………………………….

Uhusiano wake na mwanafunzi/mlezi …………………………………………………..………..

Tarehe……………………………sahihi………………………………………

2. Jina………………………………………………………

Anwani.................................................................namba ya simu……………………………… Uhusiano wake na wanafunzi/mlezi……………………………………………………………

Tarehe………………………………………

sahihi……………………………………………………………

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO, NA MAKOSA YA JINAI (KUWA MTIIFU NA MWENYE NIDHAMU KWA MUDA WOTE AWAPO CHUONI

Mimi……………………………………………………………… wa idara ya ………………………………

mwaka (darasa) ........................................................................................ ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa:

1. Nitatii sheria zote za chuo pamoja na miongozo mbalimbali itakayotolewa na viongozi kuanzia ngazi ya kiongozi wa darasa, mawaziri, serikali ya wanafunzi, wafanyakazi walio na wasio walimu na mkuu wa Taasisi.
2. Kuwa nitatimiza wajibu wangu ulionileta chuoni ambao ni kusoma na kujifunza
3. Kuwa nitahudhuria vipindi darasani na maaeneo kwa kujifunzia kwa vitendo (clinical area)
4. Kuwa nitakwepo maeneo ya mipaka ya chuo wakati wote niwapo chuoni, labda tu kwa sababu maalum na baada ya kupata ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu au mwenye dhamana ya ruhusa.
5. Nitapeleka taarifa sahihi na kwa wakati kwa mzazi/ mlezi wangu nitayopewa na uongozi wa Taasisi.
6. Ninahidi sitaenda kinyume na ahadi hii, nikienda kinyume na sheria na taratibu za Taasisi hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kufukuzwa chuo.

Jina la mwanafunzi……………………..................................…sahihi……………tarehe………….........

Jina la mzazi……………………………………………sahihi…………………tarehe……………......

Jina la msajili wa taasisi …......……………………… sahihi………………..tarehe ……………………

Jina la mkuu wa Taasisi………………………….............. sahihi ………………tarehe ………………....

MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKATOLEWA NA TAASISI

(KUKUBALI KUSHIRIKIANA NA TAASISI KUMLEA MWANAFUNZI) IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE

Jina kamili: ………………………………………………………………………………

Kazi yake: ……………………………………….....................................................

Anwani ya nyumbani: ………………………………………………………….........

Kijiji: …………………… Kata ……………………….tarafa…………………………

Wilaya………………… Mkoa……………….…... uraia……………………..............

Dini ya mzazi/mlezi ……………………………………………….........................

Dhehebu ………………………………………………………….................................

Namba ya simu ……………………………………..................................................

Nitatii wito wowote nitakaoitiwa na uongozi wa Taasisi kuhusu maendeleo ya mtoto wangu.

Ninaahidi wakati wote kushirikiana na Taasisi kusaidiana na walimu katika kumlea mtoto wangu. Nitatimiza mahitaji yake ikiwemo ada ya chuo. Juu ya hayo naelewa mwanangu akienda kinyume na sheria za Taasisi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Mimi ..........................................................Nakubali kutekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za taasisi.

Tarehe………………………………………….

Sahihi…………………………………………………………......

*** Tafadhali soma kwa umakini maelekezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kiukamilifu***

SEHEMU C: KWA MATUMIZI YA OFISI ( IJAZWE NA MSAJILI WA TAASISI SIKU YA KURIPOTI)

1. Medical examination form imejazwa vizuri

   ……………………………………………………..

2. Taarifa binafsi ya mwanafunzi imejazwa ……………………………………………………………

3. Taarifa ya binafsi ya mzazi na wadhamini imekaa vizuri ……………………………………

4. Ukiri wa mwanafunzi kufuata miongozo na taratibu za Taasisi …………………………….

5. Ukiri wa mzazi kukubali mwanae kufuata miongozo na taratibu za

   taasisi………………….